# Uimarishaji wa Ujinsuke katika Fasihi ya Kiswahili: Mifano kutoka katika Hadithi Teule za Kiswahili za Watoto

Ernesta S. Mosha


## Ikisiri

Lengo la makala hii ni kuchunguza namna hadithi za watoto za Kiswahili zinavyoweza kutumika kama njia ya kuimarisha ujinsuke[1] katika jamii ili kubadili mtazamo hasi kuhusu watoto wa kike na wanawake katika jamii ya Tanzania. Data za mjadala za makala hii zimepatikana kwa kusoma hadithi za watunzi wawili ambao ni Hua (2007) na Mwakoti (2009). Kwa kuongozwa na Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji katika uchambuzi wa data za makala hii, inabainika kuwa hadithi zinaweza kutumiwa kuwajengea watoto wa kike mtazamo chanya na uwezo wa kufanya mambo mbalimbali ili kuimarisha usawa katika jamii. Hivyo, hadithi ni njia mbadala ya kuhimiza juhudi na ubunifu kwa watoto wa kike ili kuweza kushiriki kikamilifu katika shughuli za kisiasa, kiuchumi na kijamii na kuleta mabadiliko katika mila na desturi zoeleka zinazombagua mtoto wa kike.


## 1.0 Utangulizi

Katika jamii nyingi za Kiafrika, fasihi ni sehemu muhimu ya jamii na inaakisi hali halisi, hususan kuonesha watu wanavyoishi, wanavyofikiri na kuamini. Chesaina (1995) anafafanua kuwa, fasihi ni hazina muhimu inayoonesha mambo ambayo watu wanayaamini, wanayathamini na wanayaogopa sana. Aidha, anasisitiza umuhimu wa fasihi kwa jamii anaposema:

> Fasihi ni mwakisio wa watu wanavyoishi, ni nafsi hai ya utamaduni wao. Kama kifaa cha kuhifadhi tunu za jamii, fasihi inatoa taswira na mtazamo wa wanajamii kuhusu maisha yao ya kila siku (Chesaina, 1994: 85).

Wakizungumzia uhusiano wa fasihi na jamii, Njogu na Chimerah (2008) wanaeleza kuwa msanii hawezi kujitenga na matukio yaliyo katika jamii yake. Kwa hiyo, msanii ana wajibu wa kuonesha hali halisi kwa kufichua mivutano iliyopo, changamoto na mafanikio yaliyofikiwa. Ni wazi kuwa kazi ya fasihi ina jukumu la kuwapevusha walengwa na kuwafanya wawe na mtazamo wa kuchunguza yale yanayofanyika. Kazi za fasihi zenye mwelekeo huu zinamfanya msomaji/msikilizaji kuwa na jicho la udadisi wa kuweza kukosoa, kukemea na hata kukataa mfumo unaomdhalilisha au unaomweka pembezoni (Wamitila, 2008). Fasihi inayomulika matatizo ya makundi yaliyowekwa pembezoni au kugandamizwa haina budi kuwajengea uwezo, kuwatia hamasa na kuwapa mbinu kadha wa kadha wahanga ili waweze kuondokana na hali inayowakabili. Jukumu hili la fasihi ndilo linalowasukuma wanaharakati wa kifeministi kueleza kuwa fasihi, hususan hadithi zina uwezo mkubwa wa kuwasaidia watoto wa kike na

[1] Ujinsuke ni tafsiri ya neno la Kiingereza *femininity*.

wanawake kuondokana na mifumo gandamizi pamoja na mawazo yaliyojengeka kuwa wao ni viumbe wanyonge ambao hawawezi kujitegemea au kufanya mambo makubwa ya kuleta mabadiliko (Weedon, 1997). Kazi zinazolenga kuonesha mfumo unavyowadunisha wanawake na athari zake pamoja na kuonesha wazi kuwa ukombozi wa wanawake ni ukombozi wa jamii, zinaweka wazi namna ambavyo vipera mbalimbali vya fasihi vinatumiwa ili kurithisha amali za jamii husika. Vipera hivyo ni kama vile hadithi, methali, vitendawili na nyimbo. Makala hii inatumia kipera cha hadithi katika kuchunguza usawiri wa kijinsia, hususan katika kuwaonesha watoto wa kike kuwa ni watu wanaoweza kufanya mambo ya kuisaidia jamii.

Kipera cha hadithi kimeteuliwa kutokana na kuwa na uwezo wa kuathiri namna ya kufikiri, mtazamo na hata tabia ya wasomaji (Hayakawa, 1990). Hayakawa anafafanua kuwa, wale wanaosoma hadithi nzuri siyo tu wanaweza kuishi muda mrefu kuliko wale ambao hawakusoma kazi hizo, bali pia wanakuwa na namna nyingi za kukabiliana na mambo mbalimbali wanayokutana nayo katika maisha. Anabainisha kuwa hadithi zinaweza kuleta mabadiliko makubwa katika maisha kwa kutoa mwelekeo kupitia mbinu mbadala za wahusika walio katika hadithi husika.

Akifafanua nafasi ya hadithi katika maisha ya binadamu ya kila siku, Kaufman (2012) anaeleza kuwa hadithi zinawachochea wasomaji kufikiri kama wahusika waliotumika katika hadithi na/au kufanya vitendo kama wahusika waliotumika katika hadithi hizo. Si hayo tu, bali pia husaidia wasomaji kusafiri na kupata uzoefu wa watu wengine wenye uzoefu tofauti na huwawezesha kuona mambo kwa jicho la tofauti na hata kuona jinsi watu wengine wanavyopambana na changamoto wanazokutana nazo. Kwa hiyo, wasomaji wa hadithi wanaweza kujifunza mambo mengi ambayo isingekuwa rahisi kuyaona au kukutana nayo katika maisha ya kila siku. Maoni haya ya Kaufman yanashabihiana na yale ya Cosbey (1997) anayeeleza kuwa, hadithi zinamwezesha msomaji kujifunza tabia za wahusika na sababu za wahusika hao kuwa na tabia hizo. Hali hiyo huwasaidia wasomaji kuelewa kwa undani tabia mbalimbali za watu pamoja na yale wanayokutana nayo katika maisha yao ya kila siku. Kwa maneno mengine, wasomaji wa hadithi wanaweza kujifunza tabia fulani au hata namna ya kufanya mambo tofauti ambayo hayapo katika jamii yao kutokana na wahusika waliopo katika hadithi walizosoma. Hoja hii inashadidiwa na wanaufeministi ambao wanaeleza kuwa hadithi ni chombo muhimu kinachotumiwa kusawiri upya na/au kubadili kaida za jamii zinazowagandamiza wanawake ambazo ni vigumu kuzibadilisha kwa njia ya semina na makongamano (Weedon, 1997). Maoni haya ya wanaufeministi yanaunga mkono hoja ya Ledbetter (1996) kuwa hadithi ni chanzo cha matumaini na mahimizo katika kubadilisha maisha ya mtu. Mawazo ya Ledbetter (1996) na Weedon (1997) yanaungwa mkono na Cohen (1998) anayebainisha kuwa hadithi ni nyenzo muhimu ya kudadavua yale yanayoitatiza jamii na kuweka mikakati ya jinsi ya kuyatatua. Kutokana na maelezo ya Ledbetter

(1996), Cosbey (1997), Weedon (1997), Cohen (1998) na Kaufman (2012), ni dhahiri kuwa kwa kuchunguza hadithi za watoto za Kiswahili, tunaweza kuelewa namna ambavyo tunaweza kubadili mtazamo hasi kuhusu uwezo wa mtoto wa kike na mwanamke katika jamii.

Mtazamo hasi kuhusu mwanamke ni suala ambalo limejadiliwa kwa kiasi kikubwa katika tafiti mbalimbali za fasihi (taz. Omari, 2008; Mnenuka, 2012; Mosha, 2013; Lyimo, 2014) na wanahitimisha kuwa mtazamo huo unatokana na mila na desturi ambazo zimezoeleka katika jamii. Kwa upande wa fasihi ya watoto, Lyimo (2014) anaeleza kuwa waandishi wengi bado wanawasawiri wahusika wa kike kwa kuwapa sifa za kisaguzi, ambazo kwa kiasi kikubwa zinaendeleza mtazamo hasi kuhusu mtoto wa kike. Kazi za aina hii zinaelezwa na Ngugi (2016: 84) kuwa, 'zina nafasi kubwa ya kuathiri watoto wasomaji kwa njia mbalimbali.' Ni kutokana na hoja hii Bakize (2015) anasisitiza kuwa fasihi ya watoto ni lazima ijenge mtazamo chanya na kulenga kuondoa mtazamo hasi na endapo watoto wataendelea kusoma kazi zenye mtazamo chanya kuna uwezekano wa kujenga usawa katika jamii. Makala hii inaendeleza mawazo ya Bakize (2015) kwa kuonesha umuhimu wa kutumia hadithi za Kiswahili katika kuimarisha ujinsuke. Makala imegawanyika katika sehemu sita ambazo ni: utangulizi uliotoa picha ya jumla kuhusu nafasi ya hadithi katika kuelimisha jamii, nadharia inayoongoza uchambuzi wa data, methodolojia ambapo tumetoa muhtasari wa hadithi zilizotumika, usawiri wa watoto wa kike katika hadithi teule, nafasi ya hadithi na hitimisho.

## 2.0 Kiunzi cha Nadharia

Katika kuchunguza namna ambavyo fasihi inaweza kuimarisha ujinsuke kupitia hadithi za watoto za Kiswahili, makala hii imeongozwa na Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Nadharia hii inaweka bayana namna ambavyo mitazamo pamoja na mielekeo anayokuwa nayo msomaji wa kazi ya fasihi inavyoathiri uelewa wa kazi husika. Nadharia hii inasisitiza kuwa, msomaji ana nafasi kubwa katika kuyaelewa na kuyafasiri yale anayosoma. Hoja muhimu ya Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ni kuwa msomaji anaathiriwa na yale anayosoma kutokana na tajiriba yake katika maisha (Wafula & Njogu, 2007). Kwa hiyo, msomaji anaposoma matini ya kifasihi anapata hisia na mawazo maalumu kutokana na uzoefu wake katika maisha au tajiriba yake ya usomaji. Kutokana na uzoefu au tajiriba aliyonayo msomaji, kila msomaji anaposoma kazi fulani huandika kazi yake. Rosenblatt (1995) anabainisha kuwa msomaji ni hai anaposoma matini hivyo huyafanyia kazi mawazo yanayotolewa na mwandishi katika matini husika kutokana na uzoefu na tajiriba yake. Akieleza zaidi namna msomaji anavyoweza kuifasili matini, Iser (1978) anasema kwa kawaida matini huwa haijitoshelezi kwa hiyo msomaji hulazimika kuongeza yale anayoyajua ili kuijazia matini hiyo hali ambayo inafanya awe ametengeneza matini yake akilini ambayo chanzo chake ni matini asilia aliyosoma.

Mawazo haya ya Iser yanashadidiwa na Davis na Womack (2002) wanaoeleza kuwa msomaji anaongeza kile anachoona kuwa kinafaaa katika kupata maana anaposoma kazi ya fasihi. Ni dhahiri kuwa kama msomaji akisoma taarifa zinazompa mbinu za kukabiliana na changamoto zilizopo katika jamii, atakuwa na nafasi nzuri ya kuhusisha na yale yaliyopo katika jamii yake.

Michelle (2009) anabainisha kuwa katika kupata maana ya matini, wasomaji huwa na aina mbalimbali za mwegemeo ikiwa ni pamoja na zile zinazoshabihiana na vilongo zoeleka na vilongo ibuzi. Mawazo ya Michelle yanasisistiza hoja za wananadharia ya Mwitiko wa Msomaji wanaobainisha kuwa wasomaji ni wabunifu, wapembuzi na wahakiki kila wanaposoma matini fulani (Johnson na wenzanke, 2010). Kwa upande wake, Fiske (1987) anafafanua kuwa, wasomaji wanaposoma matini fulani ya kifasihi wana uwezo wa kuamua ni yapi yanawafaa na nafasi ya matini hiyo katika maisha yao ya kila siku. Fiske anasisitiza kuwa uwezo wa wasomaji kupembua maana iliyopo katika matini unawasaidia kujua mbinu mbadala zinazoelezwa katika matini hizo ambazo zinawapa nafasi ya kuumba upya yale wanayotaka kuyabadilisha katika maisha yao. Ili kupata mabadiliko katika jamii ni lazima kuwe na vilongo mbadala vinavyowawezesha wanajamii kukataa vilongo gandamizi (Condit, 1989; Gee, 2008). Gee (2008) anafafanua kuwa, kupitia vilongo mbadala wasomaji wanatengeneza vilongo wezeshi ambavyo vinawapa nafasi ya kubadilisha mawazo zoeleka katika jamii na hivyo kuleta mabadiliko. Kwa hiyo, usomaji wa matini unaweza kumshawishi na kumhamasisha msomaji atake kugundua mambo mbalimbali ambayo yanamfaa katika maisha kupitia uzoefu na tajiriba zinazoelezwa katika matini husika. Katika makala hii tunachunguza namna hadithi za watoto za Kiswahili zinavyoweza kutumika kama njia ya kuimarisha ujinsuke katika jamii ili kubadili mtazamo zoeleka kuhusu watoto wa kike na wanawake katika jamii ya Tanzania.

## 3.0 Methodolojia

Makala hii imetumia hadithi nne za Kiswahili zinazozungumzia mtoto wa kike katika mazingira tofauti. Watunzi wa hadithi zilizotumika katika makala hii ni Mwakoti (2009) ambaye anatoka Kenya na Hau (2007) kutoka China. Hau alifanya kazi katika nchi za Tanzania na Kenya. Kwa hiyo, hadithi hizi ambazo zinatoka katika jamii hizi zinaweza kuwa chachu kwa watoto wa jamii ya Tanzania. Hadithi hizi zimeteuliwa kutokana na kuwa na wahusika watoto wa kike ambao nafasi zao zimeweka bayana uwezo na ubunifu wa mtoto wa kike na pia ndizo zilizopatikana ingawa kuna hadithi nyingine kama vile *Neema Jasiri* (Chimbalambala, 2005) na *Safari ya Mzimuni* (Mateso, 2005). Hadithi zilizoteuliwa zina wahusika watoto waliosawiriwa wakiwa na sifa chanya tofauti na zile zinazosisitiza vilongo zoeleka katika jamii. Hadithi nne tunazomakinikia ni "Msichana Aliyeokoa Watu", "Teri Waziri Mkuu wa Juba" na "Ni Nani Aliyevumbua Dau" za Enan Mwakoti zinazopatikana katika kitabu chake

kiitwacho *Msichana Aliyeokoa Watu* (2009). Hadithi nyingine ni "Watoto Jasiri" ya Sun Bao Hua kutoka katika kitabu chake *Kijana Aliyeuza Hekima na Hadithi Nyingine* (2007). Hadithi hizi nne zilisomwa na masuala yaliyozungumzia mtoto wa kike kwa njia ya wazi au isiyokuwa ya wazi yalinukuliwa. Kwa kuwa masimulizi yanajengwa kwa hadithi nzima, ili kupata mfululizo wa tukio husika, masimulizi yalichukuliwa kwa ujumla wake ili kuweza kufikia mahitimisho.

### 3.1 Muhtasari wa Hadithi Zilizotumika

Sehemu hii inaelezea kwa muhtasari hadithi ambazo tumezijadili katika makala hii. Hadithi ya kwanza ni "Msichana Aliyeokoa Watu" (Mwakoti, 2009). Hadithi hii inaeleza jinsi msichana Sidi alivyowasaidia watu wa Kimbe kutokana na madhara ya ukame. Sidi aliwazuia wananchi wasiwachinje wanyama wao kwa ajili ya kutoa sadaka kwa mungu wa mvua badala yake wachimbe visima. Baada ya mafanikio hayo, Sidi aliteuliwa na Raisi wa Kimbe kuwa mshauri katika masuala ya kilimo. Hadithi ya pili ni "Teri Waziri Mkuu wa Juba" (Mwakoti, 2009). Hadithi hii inaeleza namna msichana Teri alivyokomesha vita vya miaka mingi kati ya nchi ya Juba na Bemba. Watu wengi wa nchi ya Juba walitekwa na askari wa Bemba. Teri aliweza kuwaokoa watu wote wa Bemba waliotekwa pamoja na askari. Teri alitangazwa Waziri Mkuu wa Juba akiwa na umri wa miaka 12. Hadithi ya tatu ni "Nani Aliyevumbua Dau" (Mwakoti, 2009). Katika hadithi hii, mwandishi anaeleza jinsi wananchi wa kisiwa cha Mnazini walivyosaidiwa na msichana Chombo kwa kutengeneza dau. Chombo alitengeneza dau ambalo lilitumika kwenda katika kisiwa cha Banangwa na kwingineko kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali. Hadithi ya nne ni "Watoto Jasiri" (Hua, 2007). Hadithi hii inaeleza kuhusu watoto watatu (wavulana wawili na msichana mmoja) waliopewa maagizo na bibi kizee namna ya kupata maji ya dhahabu, ndege anayezungumza, na mti unaoimba. Wavulana walishindwa kufuata maagizo lakini mtoto wa kike alifanikiwa kufuata maagizo na kupata vitu walivyoambiwa na bibi kizee. Pia, aliwaokoa watu mbalimbali waliogeuka mawe kwa kushindwa kufuata masharti ikiwa ni pamoja na kaka zake.

## 4. 0 Usawiri wa Mtoto wa Kike katika Hadithi Teule za Kiswahili za Watoto

Hadithi za Kiswahili za watoto zilizoteuliwa zimemsawiri mtoto wa kike akiwa na sifa mbalimbali kama ifuatavyo:

### 4.1 Mtoto wa Kike ni Jasiri

Waandishi wamemsawiri mtoto wa kike kuwa ni jasiri na anafanya mambo ambayo watu wengine wameshindwa kufanya. Mwakoti (2009) katika hadithi ya "Teri Waziri Mkuu wa Juba" anaweka wazi namna Teri, mtoto wa miaka 12 alivyoonesha ujasiri wa kukabiliana na askari wa nchi ya Bemba ambao kwa muda mrefu walipigana na nchi ya Juba. Jamii inaamini kuwa watoto, hususan wa kike,

hawawezi kufanya mambo ambayo watu wazima wameshindwa. Hivyo, Teri anakumbana na upinzani mkubwa kutoka kwa Waziri Mkuu alipokwenda kuomba ruhusa ya kwenda kwa maadui zao, nchi ya Bemba, ili awaokoe watu wa Juba walioshikwa mateka ikiwa ni pamoja na mtoto wa Waziri Mkuu. Mwandishi anaonesha namna Teri alivyokabiliwa na upinzani kutoka kwa Waziri Mkuu bila kukata tamaa, anasema:

> "Nakuomba ruhusu niende kumchukua Chime (mtoto wa Waziri Mkuu) nchini Bemba". Teri alimwomba Waziri.
> "Ati kumchukua? Usinichekeshe! Mashujaa wetu wote wa kivita wameshindwa kumkomboa Chime, wewe mtoto ndiye utaweza!" Dido (Waziri Mkuu) alishangaa...
> "Nina hakika ukinipa ruhusa nitafaulu kumrudisha Chime. Tafadhali nipe ruhusa ya kwenda." Teri aliendelea kumsihi Waziri. Alipoendelea kusisitiza … aliamua kumpa ruhusa (Mwakoti, 2009: 12).

Mwandishi amemsawiri Teri kama jasiri asiyeogopa hata pale waziri alipoonesha kushangazwa na jambo alilotaka kufanya yeye akiwa mtoto, tena wa kike. Teri bila kukata tamaa aliendelea kuomba ruhusa hadi akakubaliwa kwenda katika nchi ya Bemba. Mwandishi anaweka wazi kuwa wananchi wa Juba walishangazwa siyo tu na uamuzi wa waziri lakini pia wengine walibeza kwa kuona kuwa Teri hawezi kufika popote. Mwandishi anaeleza:

> Watu walishangaa sana waliposikia kwamba Teri anaenda kumwokoa Chime. "Mtoto wa miaka kumi na miwili peke yake. Atawaweza watu hatari kama Wabemba?" Wengine waliuliza wenzao...
> Hiki kitoto hakitafika Mlima Zuwe kabla hakijazirai!" Watu wengine walisema kwa dharau (Mwakoti, 2009: 12).

Nukuu hii inaonesha kuwa watu wanadharau kuwa mtoto hawezi kufanya jambo kubwa la kumwokoa mtoto wa Waziri Mkuu na watu wengine. Pamoja na kukatishwa tamaa, Teri hakurudi nyuma aliendelea na nia yake.

Kutokana na ujasiri na kujiamini, Teri anaweza kushinda vikwazo mbalimbali na kufika katika nchi ya Bemba. Aidha, hali ya ujasiri na kujiamini inamwezesha Teri kuonana na Waziri Mkuu wa Bemba baada ya kushinda vikwazo vingi kama vile kunyimwa fursa ya kuonana na Waziri Mkuu na askari wa Bemba, lakini Teri hakukata tamaa alisisitiza kuwa alikuwa na ujumbe muhimu sana. Teri aliweka wazi kuwa kama Waziri hatafurahishwa na ujumbe huo wamuue. Ujasiri huo uliwasukuma askari wa Bemba kumpeleka Teri kwa Waziri Mkuu. Teri alimweleza Waziri Mkuu kuwa endapo watamwachilia Chime wangepata zawadi kubwa. Awali Teri alielezwa na babu yake kuwa watu wa Bemba hawajui kuhusu moto, kwa hiyo yeye alikusudia kuwafundisha namna ya kutengeneza moto na faida za kutumia moto. Kwa hiyo, Teri alipotakiwa kusema

ni zawadi gani, alimweleza Waziri Mkuu kuhusu moto na faida zake kama anavyoeleza mwandishi:

> "Moto ni kitu muhimu sana katika maisha ya binadamu. Sijui ni kwa nini nyinyi bado hamna moto. Mngekuwa na moto mngeweza kujikinga na baridi wakati wa usiku. Vilevile mngeweza kupika au kuchoma vyakula vyenu."
> "Kupika na kuchoma vyakula?" Waziri Tapa alipigwa na butwaa...
> "Ni kweli! Vyakula vikipikwa huwa vitamu sana. Nimekubali." Waziri alitamka huku akiramba vidole vyake (Mwakoti, 2009: 17-18).

Ujasiri na kujiamini kwa Teri kulifanikisha azma yake ya kuwakomboa watu wa Juba kwani baadaye Waziri Mkuu alitangaza kuwa Chime pamoja na watu wote wa Juba walioshikiliwa mateka waachiliwe huru na kwamba nchi yake haingeivamia tena Juba.

Kwa upande wa hadithi ya ''Msichana Aliyeokoa Watu'', mwandishi anatueleza kuwa msichana mdogo aliyeitwa Sidi alipinga wazo la kuwachinja wanyama wote wa nchi ya Kimbe baada ya kushauriwa na mtabiri kutoa sadaka kwa mungu wa mvua. Mwandishi anaeleza:

> …mvua imekataa kunyesha kwa sababu sadaka tunayomtolea mungu… ni ndogo sana… kila mtu achinje ng'ombe, mbuzi na kondoo wake wote ili mvua inyeshe. Watu wote isipokuwa Sidi walimuunga mkono…
> Sidi hakukubaliana na mawazo ya kuchinja mifugo wote ili kumtolea mungu sadaka. Aliona kuwa hakukuwa na haja yoyote ya mvua kunyesha halafu watu wabaki bila mnyama hata mmoja (Mwakoti, 2009: 40).

Mwandishi anaeleza kuwa wananchi wote wa Kimbe walikubali ushauri wa kuchinja wanyama wao wote ili kupata mvua, kutokana na ukweli kuwa hawakuwa na njia nyingine ya kupata mvua. Hata hivyo, ingawa watu wote walikubaliana na ushauri huo wa mtabiri, Sidi ambaye ni binti mdogo, anatofautiana na mawazo hayo, anayapinga na kushauri kuwa mvua haitakuwa na maana kama wananchi watabaki bila mifugo.

Mwandishi anafafanua zaidi kuwa Sidi alipotaka kutoa mawazo yake katika mkutano wa Wanakimbe kuwaeleza kwa nini si sahihi kuwachinja wanyama wote, hakusikilizwa. Mwandishi anaeleza kuwa, 'Watu wengi walimwona Sidi kama mwendawazimu. Hawakujua kwa nini kitoto hicho kitake kuzuia mpango wa kufanya mvua inyeshe' (Mwakoti, 2009: 42). Pamoja na Sidi kutosikilizwa, wananchi walikubaliana kuwa wasubiri wiki mbili kama mvua isiponyesha ndio wachinje mifugo yote kumtolea mungu wa mvua sadaka. Kipindi

cha wiki mbili kilichotolewa kilimpa nafasi Sidi kufikiria namna ya kuokoa wanyama wa Kimbe. Kutokana na kufikiri kwa makini aliwashawishi vijana wakachimba kisima na hatimaye wakapata maji. Kwa hiyo, wanyama wa nchi ya Kimbe walipona kutokana na ujasiri wa Sidi wa kutoa mapendekezo lakini pia kutoa mawazo mbadala ya kuchimba kisima. Mwandishi anahitimisha kwa kueleza kuwa baada ya hapo Rais wa Kimbe alimteua Sidi kuwa mshauri wake wa masuala ya kilimo.

Halikadhalika, Hau (2007) anaonesha katika hadithi ya "Watoto Jasiri" kuwa mtoto wa kike anaweza kufanya mambo ambayo watoto wa kiume, wakubwa kuliko yeye, wameshindwa kufanya. Mwandishi anafafanua namna ambavyo binti mdogo aliweza kufuata masharti waliyopewa na bikizee hivyo kupata vitu vya thamani walivyoambiwa, ingawa alikatishwa tamaa kuwa atashindwa kama kaka zake walivyoshindwa kutokana na ugumu wa masharti. Hau anabainisha binti alivyokatishwa tamaa na mwongozaji anaposema:

> "Lakini nahofia hutaweza kufanya kama vile nitakavyokuambia"…
> Unatakiwa kupanda mlima huu hadi kileleni. Ukiwa njiani utasikia matusi na vicheko, kisha utapigwa ngumi kutoka nyuma. Ukifaulu, utapata vitu vile vitatu bikizee alivyowaambia...
> Kwa ujasiri mkubwa akaupanda ule mlima. Ingawa alitukanwa na ngumi zikamwangukia mgongoni kama matone ya mvua za masika, hakugeuka nyuma. Mwishowe alikifikia kilele cha ule mlima na mara akaiona chemchemi yenye rangi ya dhahabu...
> Baada ya kupata vile vitu vitatu aliweza pia kuwaokoa ndugu zake kwa kufanya kama alivyokuwa ameelekezwa (Hau, 2007: 120-122).

Pamoja na wasiwasi aliokuwa nao mwongozaji kama ilivyooneshwa hapo juu kuwa mtoto wa kike hawezi kufanya mambo makubwa, Hau (2007) kama alivyokuwa Mwakoti (2009) amebadilisha mtazamo huo zoeleka na kudhihirisha kuwa mtoto wa kike anapopewa nafasi anaweza kufanikisha yale ambayo jamii haikutegemea.

Ujasiri wa mtoto wa kike katika hadithi hizi mbili unaweza kufananishwa na ujasiri wa Esta katika Biblia Takatifu. Yeye ingawa alijua kuwa haruhusiwi kuingia katika ua wa ndani wa mfalme bila muda wake kufika alikuwa jasiri wa kufanya hivyo ili kuwaokoa Wayahudi waliokuwa wanatakiwa kuuawa. Esta anasema, "Nitaingia kwa mfalme kinyume cha sheria, nami nikiangamia na niangamie" (Esta 4:17). Ujasiri huu wa Esta unawaokoa Wayahudi waliotakiwa kuangamizwa kwa amri ya Mfalme Ahasueri.

## 4.2 Mtoto wa Kike ni Mdadisi

Katika hadithi zilizoteuliwa, mtoto wa kike amesawiriwa kama mtu mdadisi anayechunguza kwa undani kabla hajafanya jambo lolote. Anafanya udadisi kwa kuuliza maswali mbalimbali na kupata taarifa za kina. Mwakoti (2009) katika hadithi ya "Teri Waziri Mkuu wa Juba" anatujulisha kuwa Teri alimwuliza babu yake kwa nini wananchi wa Juba wanashindwa na wananchi wa Bemba wanashinda? Babu yake alimjulisha kuwa watu wa Bemba walikuwa ni jasiri na wenye nguvu. Pia, alimweleza kuwa watu wa Juba walikuwa wanajivunia moto kitu ambacho wenzao wa Bemba hawakuwa nacho. Kutokana na udadisi wake aliweza kugundua kuwa kutokana na sifa mbalimbali zinazotokana na moto, watu wa Bemba watafaidika watakapoweza kupata moto. Hivyo, kwa kuelewa upungufu walionao watu wa Bemba, Teri alijenga hoja na kuamini kuwa atakapowaeleza kuhusu umuhimu wa moto wangemkubalia na kuweza kuwaachia watu wa Juba waliokuwa wametekwa. Kulingana na masimulizi na kama ilivyojadiliwa hapo juu, Teri alifanikiwa kuwaokoa watu wa Juba kwa kuwaeleza kuhusu umuhimu wa moto.

Katika hadithi ya "Msichana Aliyeokoa Watu", Mwakoti (2009) anatufahamisha kuwa Sidi alikuwa msichana mdadisi sana na aliweza kufikiri ni kwa namna gani anaweza kuwaokoa wanyama wasiuawe kama ilivyoelezwa hapo juu. Alijiuliza kwamba mvua inaponyesha inakwenda wapi? Je, maji yote yanapotelea wapi? Pia, alijiuliza ni kwa nini kisima cha Mungu hakikauki kama mwandishi anavyoeleza:

> Alipokumbuka kisima cha Mungu ambacho hakikauki wakati wowote, Sidi alihitimisha kwamba kulikuwa na uwezekano kwamba sehemu nyingine hasa zilizokuwa karibu na mito zilikuwa na uwezekano mkubwa wa kutoa maji zilipochimbwa...
> Sidi alikusanya vijana wote wa kijiji chake wakaanza kazi ya kuchimba maji ... Viongozi wa Kimbe waliposikia kuwa baadhi ya vijana walikuwa wameanza kuchimba maji, waliamua kuahirisha shughuli ya kuwachinja wanyama ... Zilikuwa zimebaki siku tatu wanyama wote kuchinjwa Sidi na wenzake walipofaulu kupata maji (Mwakoti, 2009: 45-46).

Kutokana na udadisi, Sidi anahusianisha yale anayoyaona na yale yanayotokea katika mazingira anayoshi – kuwapo kwa kisima ambacho hakikauki ingawa sehemu nyingine zote zimekauka. Hivyo, kujua kuwa ni lazima kuna chanzo kingine cha maji mbali na mvua. Udadisi huo unachochea maarifa zaidi na kuwashauri vijana kuungana na kuanza kuchimba kisima jambo ambalo lilizaa matunda na kuwafanya wananchi wa Kimbe wasiwachinje wanyama wao.

Aidha, katika hadithi ya "Ni Nani Aliyevumbua Dau", mwandishi anatueleza namna udadisi wa msichana aliyeitwa Chombo ulivyowasaidia

wananchi wa kisiwa cha Mnazini walioteseka kwa muda mrefu kutokana na shida ya kupata usafiri. Mwandishi anaeleza kuwa wananchi wa kisiwa cha Mnazini hawakuweza kutembeleana kutokana na tatizo la usafiri. Kwa kawaida walikuwa wanamtegemea ndege mkubwa ambaye alikuwa anafika hapo kijijini.

Chombo alibuni chombo cha kusafiria majini baada ya kugundua kuwa baadhi ya vitu vinaelea kwenye maji. Kwanza alitengeneza chombo cha majaribio kama anavyoeleza mwandishi:

> Siku iliyofuata Chombo alichonga chombo kidogo cha mti kilichofanana na bakuli la kibuyu. Alitia mawe mawili madogo ndani ya chombo hicho kisha akakirusha baharini kwa uangalifu… Chombo hicho kilielea baharini kikiwa na mawe ndani yake (Mwakoti, 2009: 33).

Mafanikio hayo yalimhamasisha sana Chombo kama mwandishi anavyofafanua: “Sasa nitatengeneza chombo kikubwa zaidi kinachoweza kuelea kwenye maji kikiwa na binadamu ndani yake” (Mwakoti, 2009: 33).

Mwandishi anaeleza kuwa, Chombo alishirikiana na ndugu yake Saumu na walifaulu kutengeneza chombo kikubwa walichokiita ‘dau’. Habari kuhusu chombo hicho cha kusafiria majini zilipelekwa kwa mfalme wa kisiwa cha Mnazini–Mfalme Teke. Mfalme pamoja na watu wa Mnazini walifurahia sana ugunduzi huo. Watu wa kisiwa cha Mnazini na visiwa vingine wakaanza kutumia dau kwenda katika visiwa mbalimbali.

Ni dhahiri kuwa Chombo alitoa mchango ambao jamii iliufurahia kwa kuwa aliweza kuiondoa jamii kutoka katika matatizo makubwa ya usafiri siyo tu jamii yake bali pia jamii nyingine ambazo zilikuwa zinategemea usafiri wa ‘ndege’. Katika hali ya kawaida ni vigumu kuelewa namna ndege anavyoweza kutumiwa kama chombo cha usafiri, hata hivyo lengo ni kuonyesha ugumu waliokuwa wanaupata wanajamii waliokuwa wanahitaji kusafiri lakini hakukuwa na njia nyingine. Ni dhahiri kuwa udadisi aliokuwa nao Chombo wa kutumia maarifa kutafuta ufumbuzi wa matatizo ya jamii, ni jambo la kusisitizwa kwa watoto katika hatua mbalimbali za ukuaji na ujifunzaji ili kuwajengea watoto uwezo wa kutoa mchango wao katika jamii.

Katika maisha ya kila siku, udadisi wa kujua ni kwa nini watu wengine wanafanikiwa katika jambo fulani na wengine wanashindwa ni muhimu sana kama Teri alivyomwuliza babu yake. Lakini jambo muhimu zaidi ni kujua wewe una kitu gani kinachokutofautisha na yule ambaye ni mshindani wako. Uelewa huo utakusaidia katika ama kujiimarisha vizuri zaidi au kutumia udhaifu wa washindani wako (kama alivyofanya Teri katika hadithi ya “Teri Waziri Mkuu wa Juba”) ili uweze kusonga mbele. Kwa upande mwingine tabia ya udadisi inakusukuma uweze kubangua bongo ili kupata namna ya kukabiliana na changamoto inayokukabili (kama alivyofanya Sidi katika hadithi ya “Msichana Aliyeokoa Watu”).

Akieleza kuhusu umuhimu wa kuwaimarisha watoto katika kuwa wadadisi, Tough (2012) katika kitabu chake cha *How Children Succeed: Grit, Curiosity, and the Hidden Power of Character*, anaeleza kuwa uwezo wa kufikiri kwa kijana unajegwa na udadisi anaokuwa nao tangu akiwa mtoto. Pia, udadisi unajengwa na mambo mbalimbali anayosoma, anayoambiwa au anayoona katika mazingira halisi. Tough anaweka wazi kuwa jamii ina nafasi kubwa ya kuendeleza udadisi wa mtoto au kukwamisha uwezo wake wa kufikiri kwa kudumaza tabia yake ya udadisi. Aidha, anasisitiza kuwa uwezo wa mtoto wa kufikiri 'hauji kimiujiza kutokana na bahati njema au karama... Ni hali inayojengwa kwa kukuza ubongo wa mtoto kwa vitu vinavyoonekana na mbinu anuwai zinazoibuliwa katika mazingira anayokulia mtoto' (Tough, 2012: 196). Hii inadhihirisha kuwa, watoto wanaposoma hadithi zinazowaonesha watoto wenzao wanavyoweza kuwa wadadisi na kuweza kuisaidia jamii ni njia mojawapo ya kuwawezesha kuwa katika nafasi ya kuanza kujiuliza maswali na kuona ni mambo gani wanaweza kusaidia au kuyapatia ufumbuzi katika familia, shule na taifa kwa ujumla.

### 4.3 Mtoto wa Kike ni Kiongozi Hodari na Mchapakazi

Mwakoti (2009) amebainisha kuwa mtoto wa kike anaweza kushika nafasi muhimu katika jamii. Katika hadithi ya "Teri Waziri Mkuu wa Juba", mwandishi anatueleza namna ambavyo Teri aliweza kupata nafasi ya juu ya uongozi kutokana na ushujaa wake aliouonesha wa kuweza kuwarejesha mateka waliokuwa wameshikiliwa katika nchi ya Bemba na kumaliza uhasama kati ya nchi za Juba na Bemba. Aidha, kupitia mhusika Teri, mwandishi anatujulisha kuwa mwanamke anaweza kufanya jamii ikapata amani na kufanya kazi na kuleta maendeleo kama mwandishi anavyosema, "Teri alikuwa Waziri Mkuu kwa miaka kumi. Chini ya uongozi wake, uchumi wa Juba ulistawi na umaskini kupungua nchini humo" (Mwakoti, 2009:21). Kuongezeka kwa uchumi wa nchi ya Juba kulitokana na uongozi imara wa Teri uliobadilisha maisha ya wananchi.

Halikadhalika, katika hadithi ya "Msichana Aliyeokoa Watu" mwandishi anatueleza kuwa baada ya juhudi za msichana Sidi kuwahamasisha vijana kuchimba visima na hivyo kuzuia wanyama wa Kimbe wasiuawe kama ilivyopangwa, alichaguliwa kuwa mshauri wa rais. Baada ya uchaguzi huo, mwandishi anasema, "Kilimo kilistawi nchini humo na Sidi akawa maarufu sana" (Mwakoti, 2009: 48). Valerio (2009) anabainisha kuwa katika utafiti uliofanyika mwaka 2004 nchini Marekani uliojulikana kama "The Bottom Line: Connecting Corporate Performance and Gender Diversity" ulionesha kuwa kampuni 500 zilizokuwa zimefanya vizuri zilikuwa na viongozi wanawake. Valerio anafafanua kuwa, ukichunguza kwa undani utagundua kwamba wanawake hao ndio waliokuwa mhimili wa mafanikio kutokana na maamuzi waliyokuwa wanafanya.

Naye, Ngaiza (2002) anatujulisha kuwa nchini Tanzania wanawake wameongezeka katika sekta rasmi za ajira kutokana na ongezeko la wanawake

wanaohitimu elimu ya sekondari, stashahada na elimu ya juu. Ngaiza anaeleza kuwa, wanawake sasa wanashiriki katika sekta mbalimbali za ajira na kushirikishwa katika uongozi. Msukumo wa wanawake kushiriki katika masuala ya uongozi umeonekana wazi katika miaka ya hivi karibuni. Kwa mfano, mwaka 2015 idadi ya mawaziri iliongezeka kutoka 14.4% kwa mwaka 2003/2005 hadi kufikia 31.27% mwaka 2013/2015. Halikadhalika, idadi ya manaibu mawaziri na makatibu wakuu wa wizara idadi ya wanawake iliongezeka kutoka 12.5% mwaka 2003/2005 hadi 40.7% mwaka 2013/2015. Kwa upande wa nafasi za juu za uongozi, wanawake wamefanikiwa kuteuliwa na kuchaguliwa katika nafasi ya Naibu Spika na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka 2015. Mafanikio haya ni makubwa sana kwa wanawake viongozi na wasomi nchini. Kuongezeka kwa idadi ya wanawake viongozi katika nafasi mbalimbali kunaonesha imani ya serikali na wananchi kwa wanawake. Pia, inaonesha kuwa jamii inaanza kuona umuhimu wa kuwatumia wanawake katika kuongoza jamii kwa kuwa mchango wao unaonekana wazi. Hata hivyo, TGNP (2015) wanatoa wito wa kuendelea kuhakikisha kuwa wanawake wengi zaidi wanajengewa uwezo ili waweze kuingia katika ngazi mbalimbali za maamuzi ili kufikia uwiano unaofaa kwa jinsi zote mbili.

Kwa upande wa ajira kwa wanawake nchini Tanzania, Muya (2014) anaeleza kwamba, katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2010–2014, pamekuwa na mabadiliko makubwa ambapo idadi ya wanawake wanaoajiriwa katika sekta rasmi na za umma wameongezeka. Mathalani, kufikia Desemba, 2014 waombaji kazi 12,858 walipangiwa vituo vya kazi na kati ya hao wanawake walikuwa 5,260 (40.9%) na wanaume wakiwa 7,598 (59.1%). Takwimu hizi zinadhihirisha ongezeko la wanawake katika nyanja mbalimbali kutokana na wanawake wasomi kuongezeka katika soko la ajira. Ongezeko la wanawake katika uongozi (Ngaiza, 2002) na katika ajira (Muya, 2014) linaashiria kuwa, endapo juhudi za wanawake zitaendelezwa kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuhamasisha usomaji wa hadithi zenye mtazamo chanya juu yao, kuna uwezekano wa wanawake kuongezeka katika nyanja za uongozi na katika ajira.

Kwa kutambua kuwa hadithi ni njia mojawapo inayotumika kuangazia yale yanayoendelea katika jamii, hadithi zinazowasawiri watoto wa kike viongozi wanaoleta mabadiliko zinaendeleza juhudi za serikali na asasi zinazohamasisha watoto wa kike na wanawake kuhakikisha kuwa wanakuwa na nafasi zinazostahili na wanashirikishwa katika masuala mbalimbali. Mwendelezo huu unathibitisha pia kuwa, wanawake wameonesha uwezo wao pale wanapofanya kazi vizuri hivyo kujenga imani na kuondoa mawazo mgando yaliyozoeleka kuwa wanawake hawawezi kushika nafasi zilizozoeleka kushikwa na wanaume.

### 4.4 Mtoto wa Kike Anamtegemea Mungu

Kumtegemea Mungu ni njia inayowajengea watu matumaini ya kupata mafanikio. Mathalani, Raisi wa awamu ya tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika

hotuba zake anasisitiza kuwa ni lazima tumtangulize Mungu katika shughuli zetu zote ili tuweze kutenda kwa haki. Mwakoti (2009) amemsawiri mtoto wa kike kama mtu anayemtegemea Mungu katika shughuli zake zote anazofanya kama anavyoeleza katika hadithi ya ‘‘Teri Waziri Mkuu wa Juba”. Anasema, ‘Kabla ya kutoka nyumbani, Teri alikuwa amemwomba Mungu huku akiangalia Mlima Zuwe. Wajuba waliamini kwamba, Mungu wao aliishi Mlima Zuwe’ (Mwatoki, 2009: 13).

Nukuu hii inaonesha kuwa hata kabla ya ujio wa dini za Kiislamu na Kikristo, Waafirka walikuwa wanaamini kwa Mungu na walimtegemea Mungu katika mambo yao waliyofanya. Nagoli (2001) anasema kuwa, Waafrika wanaamini kuwa mambo mema yanatoka kwa Mungu na wanadamu wanamwomba Mungu ili kujiweka karibu na Mungu. Nagoli anaendelea kufafanua kuwa watoto wanafundishwa kumtegemea Mungu katika kila jambo wanalofanya. Kwa hiyo, ingawa Teri alikuwa binti mdogo, aliamini kuwa ni lazima amwombe Mungu kama anataka kufanikiwa katika yale aliyotaka kuyafanya.

Kwa upande mwingine, Mwakoti (2009) anamsawiri msichana Sidi ambaye haamini kama mungu wa mvua anaweza kukubali sadaka ya mifugo yote katika nchi yao hali ambayo itafanya nchi iwe bila mnyama yoyote. Anasema:

> “Ningependa kuwaambia kwamba mimi sikubaliani na maoni ya kuchinja wanyama wote ndipo mvua inyeshe. Kwangu jambo hili halina maana kwa sababu ...” Sidi hakumalizia (Mwakoti, 2009: 41).

Jambo hili liliwakasirisha wananchi wengi waliokuwa wamekubaliana na mtazamo wa mtabiri kama anavyoeleza mwandishi:

> Unasema nini wewe? Mzee mmoja mnene aliamka kwa hasira na kumkaribia Sidi. Alitaka kumpiga Sidi lakini akazuiwa na watu waliokuwa karibu (Mwakoti, 2009: 41-42).

Pamoja na kukaripiwa vikali, Sidi hakukata tamaa alifikiri kwa makini na hatimaye aliweza kupata suluhisho la kutatua tatizo la kupata maji bila kuwaua wanyama ili kutoa sadaka kama mtabiri alivyokuwa amewaaminisha wananchi.

Katika mazingira ambayo yanaweza kuleta madhara, mwandishi anamtumia msichana mdogo kutoa elimu kuwa, mungu wa aina hiyo huenda asiwe na manufaa kwa jamii. Ingawa kama alivyobainisha mwandishi imani ni jambo gumu sana na ndiyo maana Sidi alipingwa sana na wanannchi. Hata hivyo, kupitia mtoto Sidi, mwandishi anatuhamasisha tusikate tamaa pale tunapoona jambo ambalo siyo sahihi linataka kufanyika kwa kisingizio kuwa Mungu anataka iwe hivyo. Aidha, tunatakiwa kutafakari kwa kila jambo tunalofanya kama kweli lina manufaa kwa jamii yetu hata kama linahusishwa na kumwamini Mungu kabla

hatujafanya maamuzi. Kwa njia hiyo, tutafanya maamuzi yenye tija na manufaa kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

## 5.0 Nafasi ya Hadithi kwa Watoto

Bettelheim (1976) anaeleza kuwa watoto wanatumia vyanzo mbalimbali vya taarifa kupata maana ya maisha na hadithi ni chanzo kimojawapo. Bettelheim anafafanua kuwa, kwa watoto maana ya maisha inapatikana katika hatua mbalimbali za ukuaji. Kwa hiyo, kadiri watoto wanavyopata taarifa ndivyo wanavyozidi kujifunza mambo mapya. Anasisitiza kuwa hadithi zinazowafanya watoto wajisikie kuwa wanaweza kufanya mambo tofauti na wengine huwa zinapendwa na kuigwa. Hoja hii inaungwa mkono na Strange na Leung (1999) wanaofafanua kuwa bunilizi zinazoeleza namna ya kukabiliana na changamoto, zinapendwa na watoto na vijana kwa kuwa wanajifunza namna ya kupata ufumbuzi wa matatizo mbalimbali yanayowakabili. Kwa hiyo, hadithi zilizochambuliwa katika makala hii zikitumiwa vizuri na watoto wa jamii ya Tanzania zina nafasi ya kuimarisha mbinu za watoto wa kike kujiamini na kuona kuwa wana nafasi ya kutoa mchango kwa taifa lao. Aidha, kwa kuwa hadithi hizi zinasisitiza ubunifu, zinasaidia kujenga uwezo wa watoto kutafuta mbinu mbadala kupata suluhisho pindi wanapopata changamoto. Pia, hadithi zinaweza kuwabadilisha kifikra kutoka katika kundi linalodhaniwa kuwa ni viumbe dhaifu na wasioweza kufanya mambo mbalimbali na kuwafanya wawe na fikra kuwa wanaweza.

Vilevile, hadithi tulizojadili katika makala hii zinatoa mchango katika kuwaelimisha watoto wa kike. Mathalani, zinaonesha kuwa ili mtoto aweze kupata utambulisho ni lazima afanye jambo fulani litakalomtofautisha na watoto wengine. Kwa kiasi kikubwa mtoto anaposoma hadithi kama hizi, anaanza kuwa mbunifu na kutambua mazingira yake anayoishi, changamoto zilizopo na kuanza kuwaza mchango atakaotoa katika kutatua matatizo hayo. Kwa njia hiyo, tunaweza kusema kuwa hadithi hizi zinaweza kuwa msukumo wa kujua namna ya kutafuta mbinu mbadala anapokumbana na matatizo na kujua kuwa ni lazima afikiri kila mara ili kupata suluhisho.

Jambo jingine linalopatikana katika hadithi hizi ni kuwapa sauti watoto wa kike kuwa wanaweza kubadilisha yale yaliyozoeleka katika jamii. Kwa hiyo, hadithi hizi zinawachochea watoto wa kike kuwa na mawazo mbadala na kufanya mambo kama wahusika watoto waliosawiriwa katika hadithi zilizotumika katika makala hii. Ingawa wahusika hawa wanakinzana na yale yanayosisitizwa katika jamii, ni dhahiri kuwa kama alivyoeleza Gee (2008) ni lazima kupata vilongo mbadala ili kuweza kubadilisha vilongo zoeleka. Aidha, tabia ya ujasiri na udadisi ni lazima zijengwe katika maisha ya watoto kuanzia utotoni ili waweze kujiamini na kujua kuwa wana mchango katika maisha ya kila siku hivyo kutoa mtazamo tofauti na ule uliozoeleka katika jamii kuwa watoto hasa wa kike hawana mchango katika jamii.

## 6.0 Hitimisho

Makala imeonesha kuwa hadithi zinazomsawiri mhusika mtoto wa kike kwa mtazamo chanya zinaweza kuchochea vilongo mbadala. Aidha, hadithi kama hizi zikitumiwa vizuri zina nafasi ya kubadilisha mawazo zoeleka katika jamii kuwa watoto wa kike hawana mchango katika jamii. Pia, zinaweza kutumika kama njia ya kuchochea na kuendeleza mawazo kuwa watoto wa kike wanaweza kutoa mchango katika jamii (Bakize, 2015) na ili waweze kutoa mchango huo ni lazima wazungukwe na vilongo vinavyosisitiza njia mbalimbali za kukabiliana na changamoto anazokumbana nazo. Kwa hiyo, hadithi hizi zinaweza kutumiwa kama njia ya kuwajengea watoto wa kike kujiamini na mazingira ya kujua kuwa wanaweza kuisaidia jamii yao.

## Marejeleo

Bakize, L. H. (2015). Gender Balance Struggles in Tanzanian Swahili Children's Literature. In *Kiswahili.* Pp. 59 - 66.

Bettelheim, B. (1976). *The Uses of Enchantment: The Meaning and Importance of Fairy Tales*. London: Penguin Books.

The Bible Society of Tanzania. (1994). *Biblia Takatifu*. Dodoma: The Bible Society of Tanzania.

Chesaina, C. (1994). "Images of Women in African Oral Literature: A Case Study of Kalenjin and Maasai Oral Narratives" in A. Bukenya, W. M. Kabira, and O. Okombo (eds.) *Understanding Oral Literature.* Nairobi: Nairobi University Press. Pp. 85-92.

Chinweizu, I. (1990). *Anatomy of Female Power: A Masculinist Dissection of Matriarchy*. Lagos: Pero Press.

Cohen, C. (1998). Using Narrative Fiction within Management Education. *Management Learning,* 29(2): 165-181.

Condit, C. M. (1989). The Rhetorical Limits of Polysemy. *Critical Studies in Mass Communication,* 6(2): 103–122.

Cosbey, J. (1997). Using Contemporary Fiction to Teach Family Issues. In *Teaching Sociology,* 25(3): 227-233.

Davis, T. F. & Womack, K. (2002). *Formalist Criticism and Reader-Response Theory*. New York: Palgrave.

Fiske, J. (1987). *Television Culture*. London: Routledge.

Gee, J. P. (2008). *Social Linguistics and Literacies: Ideology in Discourses* (3rd ed.). New York: Routledge.

Hayakawa, S. I. (1990). *Language in Thought and Action*. New York: Harcourt Brace.

Hau, S. B. (2007). *Kijana Aliyeuza Hekima na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Phoenix Publishers

Iser, W. (1978). *The Act of Reading: A Theory of Aesthetic Response*. Baltimore: John Hopkins University Press.

Johnson, A., de Rio, E., & Kemmitt, A. (2010). Missing the joke: A reception analysis of satirical texts. In *Communication, Culture & Critique,* 3(3): 396– 415.

Kaufman, G. F., & Libby, L. K. (2012, March 26). Changing Beliefs and Behavior Through Experience Taking. *Journal of Personality and Social Psychology*. Pp. 1-19.

Ledbetter, M. (1996).*Victims and the Postmodern Narrative, or Doing Violence to the Body: An Ethic of Reading and Writing*. New York: St. Martin’s Press Inc.

Lyimo, E.B. (2014). ‘Uchunguzi wa Usaguzi wa Kijinsia katika Vitabu vya Kiswahili vya Fasihi ya Watoto pamoja na Mtazamo wa Wadau Nchini Tanzania’. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Michelle, C. (2009). Re-contextualising audience receptions of reality TV. In *Participations*: *Journal of Audience & Reception Studies,* 6(1): 137-170.

Mnenuka, A. (2012). “Tofauti ya Dhana ya Mwanamke katika Jamii: Mifano kutoka katika Taarabu (Mipasho) na Nyimbo za Kibena.” Katika *Swahili Forum,* Kur: 19: 23-44.

Mosha, E. (2013). Textual Construction of Domestic Violence: Examples from Kiswahili Novels. In *Kiswahili,* pp. 45 -60.

Muya, M. (2014). Ripoti ya *Idara ya Ajira kutoka Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma*. Imepakuliwa tarehe 10 Machi, 2017 kutoka *www.tanzaniatoday.co.tz/News/*

Mwakoti, E. (2009). *Msichana Aliyeokoa Watu.* Nairobi: The English Press.

Nangoli, M. (2001). *No More Lies about Africa: Here’s the Truth from an African.* New York*:* AB Books.

Ngaiza, M. K (2002). ‘Gender Dynamics in Poverty Alleviation in Tanzania. Ngara District Case Study’, Unpublished PhD. Thesis, University of Dar es Salaam.

Ngugi, P.M.Y. (2016). Usawiri wa Masuala Ibuka katika Fasihi ya Watoto: Mifano kutoka Kenya. Katika *Mulika.* Kur. 76 - 86.

Njogu, K. na R. Chimerah. (2008). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Omari, S. (2008). Fasihi Simulizi na Jinsia: Mifano kutoka Nyimbo za Watoto Tanzania, *Kiswahili,* Dar es Salaam: TUKI, kur 71: 98-115.

Rosenblatt, L. M. (1995). *Literature as Exploration* (5th ed.). New York: Modern Language Association of America.

Strange, J. J., & Leung, C. C. (1999). How Anecdotal Accounts in News and Fiction can Influence Judgments of a Social Problem’s Urgency, Causes and Cures. In *Personality and Social Psychology Bulletin,* 25(4): 436-449.

Swai, E. V. (2010). *Beyond Women's Empowerment in Africa Exploring Dislocation and Agency*. New York: Palgrave Macmillan.

TGNP (2015). Uchaguzi Mkuu wa Tanzania, 2015. Katika *Jarida la Ulingo wa Jinsia*,. 4(40):10-14.

Tough, P. (2012) *How Children Succeed: Grit, Curiosity, and the Hidden Power of Character*. Boston: Houghton Mifflin.

Valerio, A. M. (2009). *Developing Women Leaders A Guide for Men and Women in Organizations.* Oxford: Blackwell Publishing.

Wafula, R. M na K. Njogu, (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Kiswahili*. Nairobi: Vide – Muwa Publisher Ltd.

Weedon, C. (1997). *Feminist Practice and PoststructuralistTheory*. Oxford: Basil Blackwell.